Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu

. . . kuwafanya watu wafahamu kile tunachojaribu kufanya. Sasa kile tunachojaribu kufanya, kumbukeni, ni kumwona Yesu Kristo akiwepo sana mpaka moyo wa kila mwaminio utachochewa, imani yake, hata atainuka na kumshikilia Mungu, na kwa ajili ya kile anachohitaji. Kwa kuwa yote tunayohitaji, katika safari hii ya maisha, yamo ndani ya Kristo.

2 Kama tu vile miti yenu hapa nje. Yote mti huo unayohitaji . . . Ni mtofaa. Hivi mliwahi kuwazia hayo? Wakati haujakuwa na urefu wa inchi moja, kila tofaa litakalowahi kuwa kwenye mti huo liko ndani yake papo hapo. Mapishi mia mara kumi, kama kuna mengi kiasi hicho; tuseme mapishi mia tano ya matofaa, kutoka kwenye mti; mapishi hayo yote mia tano yalikuwa ndani yake wakati ulipopandwa. Kama sivyo, yanatoka wapi? Mnaona? Mnaona? Wewe unaupanda tu halafu unapaswa ku—unapaswa kuvuta maji, kuyavuta kutoka ardhini. Nao hauna budi kuvuta mpaka upate mengi kupita kiwango chake, ndipo unatoa matawi, unatoa majani, unatoa maua, unatoa matofaa. Mnaona? Unayasukuma yatoke; si kuyaingiza ndani. Huyasukuma yatoke.

3 Kwa hiyo, hapo, nafikiri Kristo ni Chemichemi isiyomalizika ya Uzima. Na wakati tumepandikizwa ndani Yake, yote tufanyayo ni kunywa kutoka kwenye Chemichemi hiyo ya Uzima, na kusukuma kila kitu kitokee ambacho tunahitaji katika safari hii. Vitu vyote tunavyohitaji, viko ndani Yake. Nasi tumepandwa ndani Yake, na tunavuta kutoka Kwake, na Yeye ndiye Chemichemi isiyomalizika ya Uzima.

4 Hebu tusimame kwa miguu yetu sasa, kama mtaweza, kwa muda mfupi tu, katika uchaji, tunapolisoma Neno la Mungu.

5 Kwa ajili ya fungu letu dogo usiku wa leo, kwa kuwa kumekaribia majira ya Kwaresima, au Ijumaa Kuu, ninataka kusoma sehemu ya Injili ya Yohana Mtakatifu, kuanzia kwenye kifungu cha 12 na mlango wa 12.

> *Nayo siku ya pili yake watu wengi . . . walioijia sikukuu walisikia ya kwamba Yesu anakuja Yerusalemu;*
>
> *Wakatwaa matawi ya mitende, wakatoka nje kwenda kumlaki, . . . wakapiga makelele, Hosana! Ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana, mfalme wa Israeli!*
>
> *Naye Yesu alikuwa amepata mwana-punda, akampanda, kama vile ilivyoandikwa,*

Musiogope, mabinti *Sayuni; tazama, Mfalme wako anakuja, amepanda mwa—mwana-punda.*

Mambo hayo wanafunzi wake hawakuyafahamu hapo. . .*kwanza; lakini Yesu alipotukuzwa*. . .*ndipo* walipokumbuka *ya kwamba ameandikiwa hayo, na ya kwamba walimtendea hayo.*

Basi wakamshuhudia wale mkutano waliokuwapo pamoja naye alipomwita Lazaro. . .kutoka kwa wafu, *akamfufua.*

Na kwa sababu hiyo mkutano walikwenda kumlaki, kwa kuwa. . .*wamesikia ya kwamba ameifanya ishara hiyo.*

Basi mafarisayo wakasemezana wao kwa wao, Mwaona kwamba hamfai neno lolote; tazameni, ulimwengu umekwenda nyuma yake.

Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu.

Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya,. . .*wakamwomba wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

Filipo akaenda, akamwambia Andrea; kisha Andrea na Filipo wakamwambia Yesu.

6 Waebrania 13:8 inasema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

7 Hebu tuinamishe vichwa vyetu tunapoomba. Sasa, wakati huu wa uchaji huku vichwa vyetu vimeinamishwa, baada ya kusoma Neno hili, je! yupo yeyote humu ndani angetaka kukumbukwa katika maombi haya, na unataka Mungu akufanyie jambo fulani kwenye wakati wa mkutano huu, ama hata jioni hii? Je! ungefanya ijulikane, unapoinua mkono wako? Yeye atajua kilicho chini ya mkono wako.

8 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunalikaribia Neno Lako. Tunakaribia kwa kicho na kwa maombi, pamoja na vichwa vilivyoinamishwa na mioyo iliyoinamishwa, kwa kuwa tunajua kwamba Wewe daima ni mwaminifu kwa Neno hili. Tunaomba sasa ya kwamba Wewe utatuweka mbali na mambo na matatizo ya maisha katika ulimwengu huu, kusudi tuweze kukutumikia kwa mioyo safi na myeupe, iliyooshwa katika Damu ya Mwana-kondoo.

9 Tunakuuliza, Bwana, je! huu ndio wakati ambapo kungeweza kutokea uamsho mkuu hapa katika sehemu hii ya nchi? Kama ndio, Bwana, tupo hapa kukutumikia Wewe kwa njia yoyote tuwezayo, nasi tunajikabidhi tu Kwako, kwa ajili ya utumishi huo. Na jalia jambo fulani litendeke, Bwana, ambalo litachochea mioyo ya watu. Na huenda ikawa kwamba

mkutano huu umeandaliwa tu kwa ajili ya wachache ambao wangali wametawanyika nje kote huku, kwamba huenda ikawa ni mshiriki wa mwisho wa Mwili wa Kristo ataongezewa papa hapa Louisiana, na halafu mi—milango itafungwa. Hatujui tu kwamba ni nini, Bwana, tunasonga tu kwa uangalifu, tukichunguza kila mwenendo.

10 Pia tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utawaponya wagonjwa wote na wanaoteseka. Kama ninavyoona, amelala hapa, maskini mtoto mdogo, anayeteseka, na watu wamelala hapa, wagonjwa na wahitaji. Mungu, jalia waondoe macho yao kwenye mateso yao, usiku wa leo, na katika juma hili lijalo, na jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu wakati wa kumalizia mkutano huu.

11 Wabariki wahudumu, Bwana, na ushirikiano wao mzuri, na mambo wanayoyafanya, kujumuika pamoja. Jalia watu watambue kwamba huu ndio mo—moyo wa mchungaji wa—wao, kujaribu kuingiza kila kitu, na kila karama, na kila kitu wawezacho, kilichoadhimishwa na Mungu, kusudi kiweze kulisaidia kusanyiko lao kuona na kuamini, na kukua. Tujalie hilo, Baba.

12 Tusamehe makosa yetu. Jalia kila haja chini ya mikono hiyo, usiku wa leo. Bwana, wangu umeinuliwa, Wewe waujua moyo wangu, ni—ni maombi kwa ajili ya watu. Jalia Yesu ajulikane miongoni mwetu, Baba. Tupe kumwagika kukuu kwa baraka Zake.

13 Na tutakapoondoka hapa, usiku wa leo, jalia tuweze kusema kama wale waliotoka Emau, siku ile baada ya ufufuo, wakati tukiingia kwenye majira haya matakatifu, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu," walisema, "hapo aliposema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

14 Sio ku—kuhubiri au kuchukua muda mwingi, bali kuweka tu katika utaratibu mawazo madogo machache tu hapa sasa kabla hatujaitisha mstari wa maombi. Katika yapata dakika ishirini na tano, nadhani, nitaitisha m—mstari wa maombi, kuwaombea wagonjwa. Na sasa, kila usiku, Bw. Borders na hao watakuwa wakijaribu kuwaelezea namna, na jinsi ya kudumisha uponyaji, na kadhalika.

15 Pia, kumbukeni, hatupo hapa tukijaribu tu kuwakilisha uponyaji wa Kiungu. Tupo hapa tukimwakilisha Yesu Kristo, na ndani Yake kuna uponyaji. Na kila sifa ya Mungu imo ndani Yake. Na sisi . . . Amenunua wokovu wetu, uponyaji wetu, na yote tuliyo nayo. Nao uponyaji ni jambo dogo, na kamwe huwezi kujikita kwenye jambo dogo. Tunajua hilo. Kwa hiyo sisi ni . . . Bali tunajaribu . . . Yesu alitumia yapata asilimia themanini na sita ya huduma Yake ilikuwa juu ya uponyaji wa Kiungu, kusudi aweze kuvutia usikivu wa watu, halafu kuelezea kusudi Lake

pale lilikuwa ni nini. Na, ni jambo lile lile, tunajaribu kuendeleza huduma Yake katika njia nzuri zaidi tujuayo, tukiamini kwamba angali anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.

16 Sasa, tunajua kwamba, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Hivyo basi, Mungu na Neno Lake ni kitu kile kile. Ni Mungu katika maandishi. Wewe si zaidi ya neno lako. Mungu si zaidi ya Neno Lake.

17 Kwa hiyo karamu hii kuu tunayoikaribia hapa katika majira haya, wakati huu wa Kwaresima, jinsi wanavyouita, na kuikaribia Ijumaa Kuu, na—na halafu Jumapili ya Pasaka, juma moja kabla ya Jumapili ya Pasaka, ninaamini. Kwa hiyo tunakaribia haya. Niliwazia ningesoma Andiko hili, ambapo Wayunani hawa wenye mioyo yenye njaa walikuja kuabudu kwenye sikukuu ya Pasaka. Nao hawakujua kuwa huyo alikuwa ndiye Mwana-kondoo wa Pasaka, Kristo alipaswa kuwa.

18 Lakini mioyo yao ilikuwa na njaa. Walitaka kumwona. Walikuwa wamesikia mengi sana kumhusu, na kujua kwamba mambo makuu walikuwa wamesikia ambayo Yeye alikuwa amefanya. Basi kwa hiyo hapana shaka, wakija kwenye sikukuu, lazima walikuwa wamesoma mengi katika Maandiko juu ya kile Yeye alicho, na tabia Ya—Yake, na kile ambacho angefanya wakati akija. Kwa hiyo walitaka kuona.

19 Waliwajia wanafunzi Wake, nao wakapewa majaliwa ya kumwona Yeye, kwa hi—hisani na huduma ya wanafunzi Wake. Waliletwa katika Uwepo Wake, na watumishi Wake.

20 Na sasa kama Waebrania 13:8 inasema, kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," nami nina hakika kwamba hapa kwenye—kwenye . . . katika Baton Rouge, kwamba tuna shauku tu ya kumwona Yesu kama walivyokuwa nayo kumwona wakati ule. Mimi . . . Kila mtu aliye na akili timamu, na kusikia habari za Bwana Yesu, hutamani kumwona.

21 Loo, niliposikia habari Zake mara ya kwanza, nilipokuwa mvulana, ni—ni—nisingeweza kabisa kuvumilia. Niliwazia, "Kama Yeye ni Mungu, Yeye—Yeye daima alikuwa ni Mungu, Yeye—Yeye daima atakuwa ni Mungu."

22 Kwa hiyo kujaribu kuiweka mbali katika wakati fulani mkuu uliopita, ama—ama wakati fulani mkuu unaokuja, hiyo tu ni tabia ya mwanadamu. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, akitazamia yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya. Hiyo tu ni tabia ya mwanadamu. Daima imekuwa hivyo, na ingali inabaki hivyo, usiku wa leo.

23 Lakini, sasa, Wayunani hawa walitaka kumwona, nasi tunataka kumwona. Vema, sasa, kama Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, na si . . . Yeye hajafa. Yu hai. Na kama Yu hai, kama Maandiko yanavyodai kwamba Yu hai, basi ni kwa nini hatuwezi

kumwona? Tuna haki ya kuuliza kumwona. Kumbukeni, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, nyinyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu. Ulimwengu hautaniona, bali ninyi mtaniona." Na sasa ikiwa Yeye ni yule jana, leo, na hata milele, basi ni kwa nini tusingeweza kumwona?

24 Sasa kama ningeenda kwenye mawazo mbali mbali ambayo tumekuwa nayo. Pia kumbukeni ya kwamba Mungu kamwe hafanyi jambo lolote nje ya yale aliyoahidi kufanya. Mnaona, Yeye daima hutoa ahadi, halafu anakuja kuitimiza.

25 Mungu, hapo mwanzo, akijua mwisho tangu mwa-. . . mwanzo, maana Yeye alikuwa asiye na kikomo. Sote tunajua hilo. Yeye yuko kila mahali, yuna nguvu zote, na hana kikomo. Sasa, ikiwa Yeye hana kikomo, basi alijua mambo yote, na sasa . . . na anajua yote.

26 Kwa hiyo angalia, basi, Yeye aligawa Maandio Yake kote kupitia vizazi vijavyo. Ndipo basi wakati huu ukiisha, mbona, daima sisi hujaribu ku—kuwazia mambo jinsi tunavyofikiri ni sahihi, lakini kila mara . . . Kama Mungu ametoa ahadi kwa ajili ya wakati huo, njia Yake ya kawaida ya kufanya chochote, wala habadilishi kufanya hivyo.

27 Kumbukeni, Mungu kamwe habadiliki, habadilishi njia Zake. Kwa kuwa hiyo ndiyo sababu tunaweza kuweka imani yetu kwa hakika katika kile Mungu alichosema kuwa Kweli, Biblia. Sasa inakubidi kumweka Mungu mahali fulani.

28 Sasa, kama Mungu alikuwa anaenda kuuhukumu ulimwengu, na anaenda kuuhukumu. Kama tungesema, kama ningewaambia Wakatoliki ya Kifaransa, mnafikiri atauhukumu kwa kitu gani? "Kanisa Katoliki ya Kifaransa." Katoliki ya Rumi inaamini atauhukumu kwa kanisa hilo. Othodoksi, Wakatoliki wa Kiothodoksi ya Kiyunani, wanaamini kwamba atahukumu kwa hilo. Wamethodisti wangesema, "Kanisa letu." Wabaptisti, "Kanisa letu." "Wapentekoste!" Mnaona, lingekuwa jambo la kutatanisha sana, hata mtu asingejua la kufanya.

29 Lakini Yeye alisema atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, naye Yesu Kristo ni Neno, kwa hiyo Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Neno. Sasa, Biblia ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. *Huu* ndio ufunuo. Hakuna kitu cha kuongezwa Kwake au kuondolewa Kwake. Hicho hicho kitaondolewa, sehemu yetu, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima, kama tukiongeza au kuondoa Kwake. Hilo ndilo Neno la Mungu, nasi tunaliamini.

30 Sasa, kila kizazi, wakati kanisa kwa kawaida hulichanganyisha sana na kila kitu, mpaka, wakati ukiwadia kwa Neno kutimizwa, wanaangalia nyuma kwenye kizazi kingine huko nyuma kabisa, kilichofanyika nyuma kabisa katika siku nyingine, na wanakosa kuona kilichofanyika katika siku hiyo.

31 Sasa kwenu enyi Wakatoliki, jinsi mlivyowakosa wale watakatifu. Vipi kuhusu Joan wa Arc, M—Mfaransa? Labda tu niinue hilo, kwa sababu himaya ya Kifaransa. Kumbukeni, kasisi alimchoma moto kwa ajili ya imani, kama mchawi. “Alikuwa ni mchawi,” ati kwa sababu msichana huyo alikuwa wa kiroho. Aliona maono, na kadhalika, nanyi mlimchoma moto kuwa ni mchawi. Halafu, baada ya kitambo, mlipoona makosa yenu, mliifukua miili ya makasisi hao na kuitupa mtoni, kwa ajili ya toba. Lakini, mnaona, imepita tayari.

32 Na hivyo ndivyo ilivyo daima. Hutupita wala hatuitambui.

33 Hata kwa wanafunzi, Yesu alisema, wakati mmoja akizungumza nao. Walisema, “Ni kwa nini wa—waandishi wakasema kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?”

34 Akasema, “Amekuja tayari, wala hamkumjua.” Ndipo wakafahamu kwamba ilikuwa ni Yohana Mbatizaji. Hata hao wanafunzi, ile sauti nyikani, na Malaki 3 ikitimizwa, mbona, iliwapita moja kwa moja na hata hawakuielewa hata kidogo. Mnaona?

35 Na inawezekana kwamba tunaweza kuiacha itupite, na tukose kuiona. Njia ya Mungu daima . . .

36 Sasa kama ingekuja katika mfumo mzima, ama dhehebu fulani, kama vile Protestanti, Methodisti, Baptisti, Pentekoste, au baadhi ya madhehebu yao yangezalisha hiyo, wangeiamini. Vema, basi, wengine wasingekuwa na uhusiano nayo.

37 Kwa hiyo Mungu kamwe hafanyi kazi, katika wakati kama huu, na dhehebu lolote. Hajawahi kufanya hivyo. Yeye daima hufanya kazi na mtu binafsi, mtu mmoja, wewe, huyo mtu mmoja tu. Ni wewe, kati yako na Mungu, si kati ya dhehebu lako na Mungu; kati yako wewe, kama mtu binafsi. Mungu daima huifanya namna hiyo, daima amefanya hivyo.

38 Na sasa Biblia ilisema, “Yeye hatendi lolote asipowafunulia manabii Wake, watumishi Wake hao manabii.” Na daima, sana kama katika wakati wa Eliya, na wakati wa Musa, na nyakati hizo mbalimbali, Yeye angelifunua.

39 Sasa ilikuwa imeandikwa kwenye Maandiko kwamba ninii . . . Mungu alikuwa anaenda kuwapa ishara kuu, ishara kuu, ishara ya milele, “bikira alikuwa anaenda kuchukua mimba.” Halafu basi kulikuwa kunaenda kuwapo na Mmoja atakayezaliwa, Mtoto, tulimjua kuwa ni Masihi. Maandiko yote, kote kuanzia Mwanzo, kuendelea, yalikuwa yameungana katika kuja kwa Masihi.

40 Manabii walikuwa ni sehemu ya Neno. Yesu alisema waliitwa ‘miungu.’ Na ndivyo walivyokuwa, mradi Neno la Mungu lililetwa kwao. Alisema, “Mwawezaje kunihukumu ninaposema kuwa Mimi ni Mwana wa Mungu? Na—na, nyinyi, wale . . . Imeandikwa katika torati yenu, ‘wale ambao Neno la

Bwana huwajia,' mliwaita miungu.'" Mnaona, ninii . . . Haikuwa manabii; ilikuwa ni Neno la Mungu. Na ni kitu kile kile wakati huu. Na ilikuwa ni Yesu, kitu kile kile, Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na hilo daima ndilo Nuru ya wakati.

41 Sasa kama tungeangalia kote, usiku wa leo, na tungerudi nyuma kwenye baadhi ya haya makanisa makuu, kote kupitia kwenye wakati, na kusema, "*hili* ndilo, *hili* ndilo," msipokuwa waangalifu, tutakuwa tunatembea katika mng'ao badala ya Nuru. Tunaangalia kwenye kitu kilichopita, miaka iliyopita, tukiangalia nyuma.

42 Mtu yeyote anayeendesha motokaa kwenye barabara, akiangalia kupitia kioo cha kuangalia nyuma, ataangamia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Unachukua kwa mfano baadhi ya dada zetu wanaojaribu, umri wa miaka hamsini, wanajaribu kuonekana wenye umri wa miaka kumi na sita. Unaona, unaangalia nyuma.

43 Angalia mbele! Angalia kule unakoenda. Angalia kule unakoenda, si kile ulichotoka kwacho. Paulo alisema, "Tukiyasahau mambo yaliyopita, nakaza mwendo kuifikia mede ya wito katika Kristo." Huna budi daima kuangalia kule unakoelekea, si kule ulikokuwa.

44 Ukikaza macho kwenye kioo cha kuangalia nyuma, hivi karibuni utaangamia. Hilo limekuwa ndilo tatizo. Hiyo ndiyo sababu Luther aliangamia wakati nuru ya Wesley ilipotokea. Hiyo ndiyo sababu Wesley aliangamia—aliangamia wakati Wapentekoste walipotokea. Na tusipokuwa waangalifu, Wapentekoste wanaenda kuangamia, pia, ikiwa hawatakaa chonjo, kuangalia. Unaona, daima unaangalia nyuma, ukirejelea kitu ambacho mtu fulani alifanya huko nyuma. Wakati sisi . . .

45 Wakati, tumeamrishwa kuangalia mbele, endelea kusonga mbele. Unabii wa—wao ulitimia katika siku zao, huu unatimia katika siku hii, na unaofuata unatimia katika siku inayofuata. Imegawanywa, hadi wakati wa mwisho. Na kuna mambo yanayopaswa kuwa yakiendelea sasa, kulingana na Maandiko, Roho Mtakatifu duniani, akimiminwa juu ya watu.

46 Sasa, wakati Yesu alipokuja, hao Waandishi na wengine walipaswa kumtambua, bali hawakumtambua, kwa kuwa walikuwa wameimarika sana katika mapokeo yao. Mafarisayo, Masadukayo, Waherodia, chochote kile, walikuwa katika mapokeo hayo, wamebobea sana, mpaka unabii wenyewe wa Kristo Mwenyewe, kile ambacho alipaswa kuwa, walikosa kuuona. Aliwaambia, kasema, "Yachunguzeni Maandiko, maana katika Hayo mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

Wakasema, "Sisi ni wanafunzi wa Musa."

47 Akasema, “Kama mngalikuwa wanafunzi wa Musa, mngalinijua Mimi, maana Musa aliandika kunihusu. ‘Bwana Mungu wenu atamwinua Nabii mithili yangu.’”

48 Walidai kuwa, bali hawakuwa, kwa sababu walikuwa wamebobea sana katika mapokeo. Sasa, hivyo ndivyo walivyokosa kumwona katika siku hiyo waliyoishi. Sasa, hiyo ingeweza kujirudia, mwajua. Daima imejirudia, na inaweza kujirudia tena.

49 Sasa hebu turudi nyuma kwa dakika chache tu. Na njia ya pekee ya sisi kuweza kujua kile alicho Yeye . . .

50 Sasa, leo hii, kama tukichukua mtu wa kawaida, kile Kristo anachopaswa kuwa, sisi . . . Baadhi yao humwelezea kama kitu fulani kikuu, cha kihistoria. Wengine humshusha kuwa mtu tu wa kawaida. Na wengine humfanya kuwa mwanafalsafa, nabii, ama—ama kitu fulani, kingine namna hiyo, mtu mwema, mwalimu.

51 Lakini Yeye, chochote alichokuwa, Yeye angali hicho, kulingana na Maandiko. Mnaona? Sasa kama tungeenda huko mjini, kumtafuta, na twende—twende tukiangalia kote, kuona iwapo . . . Sasa, kumbukeni, ahadi Yake ni kwamba Yeye angekuwa pamoja nasi.

52 Sasa kama tulienda kumtafuta mtu fulani kwenye . . . tungesema . . . ningesema, labda, “Awe na urefu wa futi sita.” Nawe ungesema, “La, ingekuwa saba na nusu.” Mwingine aseme, “La, alikuwa futi nne tu; alikuwa ni jamaa mdogo.” Unaona, sote tungechanganyikiwa.

53 Vema, wangesema, “Labda angekuwa na makovu ya msumari mkononi Mwake.” Mnafiki yeyote tu angeweza kuwa na makovu ya msumari mikononi mwao, na alama za miiba. Na, hata hivyo, Yesu ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu. Lakini tungejuaje kuwa Yeye alikuwa ni Nani?

54 Hawakumjua wakati ule kwa sababu ya vazi lake. Kwa sababu, Yeye alitembea moja kwa moja miongoni mwao, hata baada ya kufufuka Kwake. Naye angetembea pamoja nao, na bado hawakumtambua. Mnaona? Haikuwa ni vazi Lake. Alivalia tu kama mtu mwingine yeyote. Haikuwa ni vazi Lake. Haikuwa ni namna Yake. Haikuwa ni dhehebu Lake. Haikuwa ni kadi Yake ya ushirika aliyoibeba, maana hakuwa nayo. Kwa kweli, hakukubaliana nayo, kwa hiyo haikuwa ni hiyo.

Wakasema, “Hatujui alikotoka.”

55 Ndipo yule aliyekuwa kipofu akasema, “Hilo ni jambo la kushangaza. Wewe ni kiongozi wa siku hizi, na Yeye ameyafumbua macho yangu, na wewe hata hujui alikotoka.” Alikuwa na theolojia nzuri ya aina yake. Mnaona? Akasema, “Hamjui yale aliyofanya mtu huyu, mambo aliyofanya, na hata hivyo mnategemewa kuwa ndio viongozi wa leo.” Sasa . . .

Lakini sehemu ya kuhuzunisha, kwao, macho yao yalipofushwa. Ilipaswa kuwa hivyo.

56 Je! mlijua kwamba kanisa linapaswa kuwa hivyo, katika siku za mwisho, pia? "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wakiwa na mfano wa utauwa bali wakikana Nguvu zake. Kutoka. . . " Huo ni unabii ule ule, kitu kile kile. Hakika ndivyo. Katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, Yesu alikuwa nje ya kanisa, akijaribu kurudi ndani, akibisha mlangoni. Wakati pekee aliopata kuwekwa nje ya kanisa, ni katika Wakati wa Laodikia tunaoishi sasa. Kwa hiyo tunaona tumerudi tena mahali tulipoanzia.

57 Sasa, njia ya pekee ya kweli ya kujua kile Yeye alichokuwa, ama kile alicho, ni kutafuta kujua kile alichokuwa, sasa, maana angekuwa ni Yeye yule. Sasa hebu turudi tu nyuma na kuvuta mambo machache ambayo Yeye alifanya. Sote tunajua kuzaliwa Kwake na bikira, na hatutaanza na hilo.

58 Lakini nilisoma kutoka kwa Yohana Mtakatifu. Hebu turudi nyuma kwa Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, na tuone tu kile alichokuwa, ndipo basi tunaweza kuelewa kile Yeye—kile Yeye alicho sasa. Chochote kile alichokuwa wakati ule, Yeye ni kitu hicho hicho sasa. Vema. Sasa tunaona hapa, hapo mwanzo, alikuwa ni Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno." Basi angali ni Neno. Mnaona? Mnaona? A-ha. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Vema.

59 Wakati ule, hicho ndicho alichokuwa wakati ule, alikuwa ni ahadi iliyothibitishwa ya Mungu kwa ajili ya wakati huo. Hiyo ilimfanya Neno. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, atakuwa ni kitu kile kile leo, Neno tena. Mnaona? Na Yeye—Yeye—Yeye—Yeye aliwaambia kuangalia hicho. Hicho ndicho alichokuwa. Alikuwa Neno. Neno lilifanyika mwili. Hicho ndicho alichokuwa. Sasa, alipofanyika Neno, naye Mungu akashuka chini katika umbo la Roho Mtakatifu, katika mfano wa hua, na kuenda juu Yake, na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake."

60 Ndipo tunaona kwamba, huduma Yake ilianza, maombi kwa ajili ya wagonjwa, uponyaji. Kila mtu alimpenda. Alikuwa mzuri, alijulikana kuwa ni Jamaa mzuri. Halafu basi, akiwa katika huduma Yake ya kwanza, kile kilichomtambulisha . . .

61 Kumbukeni, Wayahudi daima waliamini uponyaji wa Kiungu. Walikuwa na birika kwenye lango hapa, la Bethsaida, Bethesda, kwenye lango, lango zuri. Watu walikaa pale, umati wa—wa watu wanyonge ambao ni walemavu, viwete, vipofu, na wakaingia kwa maji kwa ajili ya kuponywa.

62 Mungu daima ameandaa njia kwa ajili ya uponyaji, kwa hiyo uponyaji Wake haukuwa hasa kilichowavutia Kwake. Kulikuwepo na kitu cha ziada kilichouvutia usikivu wake.

63 Sasa tunaona ya kwamba iwapo. . .kile alichopaswa kuwa, Musa alikuwa amesema kile alichopaswa kuwa, nao manabii wote walikuwa wamenena habari Zake, sasa hana budi kutambulishwa ha hilo.

64 Sasa hiki hapa kile alicho, Neno. Sasa, Waebrania, mlango wa 4, inasema kwamba, "Neno la Mungu lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili. Ndivyo lilivyo, hukata hata kwenye mafuta yaliyomo kwenye mfupa, na huyatambua mawazo yaliyoko moyoni." Hivyo ndivyo Neno lilivyo.

65 Sasa, unaona, Neno lilipowajia manabii, walitambulishwa kwa unabii wao. Mungu alisema, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitanena naye katika maono, na ku. . .na kumwonyesha ndoto, na kadhalika." Kwa maneno mengine, "kufasiri ndoto," kama vile Yusufu na hao wengine walivyofanya. Na huo utakuwa utambulisho wake. Na basi huo ndio utambulisho aliokuwa nao, Neno lililovuviwa, kwa ufunuo, mnaona, Neno lililopaswa kutimizwa. Unabii wake ulimtambulisha kuwa nabii, "Nalo Neno humjia nabii."

66 Kwa hiyo wakati Yesu alipokuja jukwaani, Biblia ilisema alipaswa kuwa Nabii. Musa alisema, "Bwana Mungu wako atamwinua Nabii mithili yangu." Na Israeli daima waliamini manabii wao, kwa sababu huyo alikuwa ni Mungu akijitambulisha Mwenyewe ndani ya wanadamu, daima. Msomaji yeyote wa Biblia anajua hilo. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe, ilikuwa ni katika manabii Wake. Walikuwa tu ni watu wa kawaida. Bila shaka, walizaliwa kwa kusudi hilo.

67 Kama tunavyojua, kuna karama za mahali pamoja, za karama tisa katika kanisa. Bali kuna ofisi za Kanisa, na hizo, Mungu, zilizokusudiwa kimbele, ama zilizochaguliwa kimbele, "Mungu ameweka Kanisani: mitume, halafu manabii, na walimu, wachungaji, wainjilisti," na kadhalika, hizo ni karama za Mungu zilizowekwa Kanisani. Halafu kuna karama tisa za kiroho ambazo hufanya kazi katika mwili wa mahali pamoja, na wa waaminio, na hazina budi kupimwa na waamuzi wawili au watatu kabla hazijaletwa kwa kanisa, maana wakati mwingine huenda zikakosea.

68 Lakini waangalie hawa manabii, walivyozaliwa, kama vile katika. . .naamini, katika Yeremia hapa, Mungu alisema, "Kabla hata hujachukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mama yako, nilikuchagua kuwa nabii juu ya mataifa." Mnaona? Musa alizaliwa nabii. Naye Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na mbili kabla hajazaliwa, "yeye alikuwa ndiye sauti ya mtu aliaye nyikani," Isaya nabii akinena juu yake. Unaona,

si...Karama hizi ni karama za kuzaliwa, Mungu akiziweka Kanisani.

69 Na, sasa, na wakati wa kuja kwa kwanza kwa Bwana wetu, hakukuwa kumekuwa na nabii duniani kwa miaka mia nne. Malaki alikuwa ndiye nabii wa mwisho, naye alinena kuhusu kuja kwa Yohana. Katika mlango wa 3 wa Mathayo, ambaye angekuwa ni Isaya—Isaya, nabii, alinena habari zake. Halafu basi, pia, ndipo Malaki akanena na kusema Eliya angejitokeza uwanjani, mmoja anayemtangulia Kristo. "Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kutayarisha njia," kama alivyosema katika Mathayo 11, akimtambulisha Yohana.

70 Na kitu cha ajabu sasa, wakati Yesu alipoanza kunena, na alikuwa akijitambulisha Mwenyewe, hebu tuangalie jinsi alivyofanya hilo sasa. Kama Yeye si wa Kimaandiko katika yale aliyofanya, basi hakuwa Masihi. Hana budi kuja kulingana na Maandiko.

71 Sasa kulikuwako na mtu jina lake Andrea, alikuwa akihudhuria uamsho wa Yohana, ambapo Yohana alisema Yeye alikuwa yuaja. Yeye ni...Yohana alikuwa na hakika sana na kuja Kwake, akasema, "Amesimama moja kwa moja miongoni mwenu sasa," maana alijua kwamba ilimpasa kumtangaza huyo Masihi.

72 Sasa, kamwe hakuenda kwenye seminari, kujifunza kile Masihi anachopaswa kuwa. Alienda nyikani, na alikuwa huko nje peke yake, kisha akaja. Maana, alikuwa...alikuwa asifunzwe na binadamu. Ilibidi afunzwe na Mungu. Kwa sababu, sasa, baba yake alikuwa ni kuhani, na ilikuwa ni desturi kwamba mwana alifuata ka—kazi ya baba na elimu yake, na kadhalika. Lakini kazi ya Yohana ilikuwa kuu sana, muhimu sana.

73 Vema, wengi wa watu hao, alisema, "Sasa, mnajua Ndugu *Fulani-wa fulani* hapa, yeye anazo zile—zile sifa."

74 Bali Yohana alienda huko nje nyikani, na, mpaka, alikuwa pamoja na Mungu mpaka akajua kikamilifu kile ishara ya Masihi ingekuwa. Wakati alipokuja, alisema, "Sikumjua, lakini Yeye aliyesema, 'Yule ambaye utamwona Roho akishuka juu Yake, na kukaa, Huyo Ndiye ambaye atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.'" Mnaona? Alijua na alikuwa na hakika kabisa kwamba huyo alikuwa Ndiye.

75 Sasa, Andrea alikuwa akijaribu kumleta ndugu yake, Simoni. Walikuwa ni wavuvi, nao walikuwa wakijaribu kumfanya ndugu yake kuja kwenye mkutano.

76 Sasa, nilisoma hadithi wakati fulani uliopita kuhusu maisha yao. Walikuwa ni waaminio kwelikweli katika dini ya Mafarisayo. Naye alikuwa na—na...Baba yake, baba yake jina lake Yona, naye alikuwa ni—alikuwa ni mvuvi mashuhuri, pia. Na, mara nyingi, ingewabidi kumtumainia Mungu kwa ajili ya chakula chao, samaki wao, kulipa madeni, na—na kupata

chakula. Nami, nikisoma siku moja ambapo huyo baba mkongwe alimchukua Simoni na kumketisha chini, na yeye pamoja na Andrea, ndipo akasema, "Enyi wavulana, siku zote niliamini kwamba ningeishi kuona kule kuja kwa Masihi, ambaye tumemtazamia, miaka hii yote. Na sasa, wanangu, kabla Masihi hajaja, labda nitakuwa—nitakuwa nimeondoka, kwa kuwa mimi ni mkongwe. Lakini siwatakeni ninyi wavulana kudanganyika. Sasa kutakuwa na kila namna ya mambo yatakayoinuka kabla hajaja."

77 Inabidi kuwa hivyo daima, mwajua, ili kwa namna fulani kuondolea mbali kitu ha—halisi inapofikia hapo. Mnaona, Shetani daima yuko huko nje. Kama tu vile kabla ya Yesu kuja, walisema kulikuwako na Yesu wengine walioinuka na kupeleka makundi nyikani, wakaangamia, na kadhalika.

78 Bali alisema, "Wanangu, kumbukeni, Masihi huyu atatambulishwa Kimaandiko." Loo, jinsi anavyopaswa kuwafundisha watu leo hii! Mnaona? "Masihi atatambulishwa na Maandiko, kwa sababu Musa alisema kuwa Bwana Mungu wetu atamwinua nabii mithili yake. Naye Musa ni kiongozi wetu, nasi tunatazamia. Sasa, imekuwa mamia ya miaka, hatujakuwa na nabii yeyote, bali Musa alisema kwamba Mmoja alikuwa yuaja. Na, bila shaka, kwamba kiungo hiki hapa pasipo nabii kimekuwa ili kutambu-. . .kutambulisha kwamba wakati kitakapokuja, Yeye atakuwa na sifa za huyo nabii." Sote tunafahamu Andiko hilo.

79 Sasa tunaona kwamba, baadaye, kwamba Yesu alikuwa hajaonyesha ishara yoyote bado. Siku moja, Simoni akaja katika Uwepo Wake, pengine, akiwa na shaka kidogo, juu ya ushuhuda wa Andrea, kwa kuwa alikuwa amesikia yote haya yakitendeka kumhusu mtu huyu wa mwituni, akiwazamisha watu huko chini mtoni, pamoja na mabatizo, na kadhalika. Naye asingeweza kuendea hilo, maana kulikuwa na upuuzi mwingi sana uliokuwa umepitia Palestina, wakati huo.

80 Lakini, siku moja, Simoni alikuja katika Uwepo wa Bwana Yesu. Sasa hebu tuangalie kile alichokuwa jana, kwa hiyo mbegu teule, yule Simoni aliyekusudiwa mahali hapa, ile mbegu. Kwamba kama . . .

81 Hapo mwanzo, Mungu hata hakuwa ni Mungu. Alikuwa ni yule mkuu wa Milele, na humo ndani mlikuwamo na sifa. Sifa zilikuwa ni mawazo Yake. Na ndipo akawa Neno, namna hii. Nalo Neno likitamkwa . . . Vema, wazo likidhihirishwa, ni Neno. Neno, likitamkwa, ni wazo.

82 Halafu basi, kumbukeni, kama uliwahi kuwa katika wazo la Mungu, daima utakuwa humo. Kama una Uzima wa Milele, wewe ni dhihirisho, ama sifa, ya wazo Lake kwa wakati huu. La sivyo, wewe . . . Kuna Uzima wa Milele mmoja tu, na Huo umekuwapo daima. Na wewe, katika mawazo Yake,

ulikuwapo kabla ya ulimwengu kuwepo. Hiyo ndiyo sababu alisema Yeye alikuchagua "kabla ya msingi wa ulimwengu." Si kile tunachowazia, kile mtu mwingine anachowazia. Ni kile ambacho Mungu, wa Milele! Daima ulikuwepo, unaona, katika mawazo Yake.

83 Ilikuwa ndani Yake kufanyika mwanadamu, hiyo ndiyo sababu Kristo alikuwa ndiyo sura iliyodhihirishwa. Mnaona? Sasa, alikuwa awe Baba, alikuwa awe Mwana, alikuwa awe Mwokozi, alikuwa awe Mponyaji. Hakukuwa na chochote, hakukuwepo hata na Malaika, wala chochote. Ndipo, akawaumba Malaika, ndipo akawa Mungu, akaabudiwa. Basi haya ni madhihirisho ya mawazo Yake.

84 Hakuna kosa. Kila kitu kitatokea sawa. Usitishwe. Saa kubwa ya Mungu inasonga moja kwa moja. Itakuwepo, itakuwa na Kanisa lisilo na doa wala kunyanzi. Lilikuwa katika mawazo Yake. Jambo ni kwamba, je! niko Humo ndani, je! uko Humo ndani?

85 Naye Huyu hapa, wazo la Milele la Mungu, likidhihirishwa katika Uwana. Loo, jamani! Huyo hapo Mungu, Imanueli, wakati huo. Angalia, basi, Yeye alikuwa ni Neno. Sasa hapa . . .

86 Je! ninawaziba masikio? Simaanishi kuwapigia makelele. Wakati mwingine sisi huzungumza nje kwenye viwanja vikubwa na kadhalika, nami sikusudii kunena kwa sauti kubwa kupita kiasi. Sasa hebu ninii . . . Yeyote yule anayeidhibiti, wanipunguzie kidogo, wakiweza, kama ikiwa kubwa sana.

87 Sasa angalia, katika hili, wakati Yesu alipokuja, huyu hapa akaja Simoni, akitembea mbele Zake. Na mara tu Yesu alipomwona, akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona."

88 Loo, je! hiyo iliutia moto moyo wa mvuvi huyo! Hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, hakuwa na elimu, bali alijua kwamba hilo lilikuwa ni Neno kwa sababu liliyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwake. Huyo hapo alikuwa ni Masihi. Ingawa Biblia ilisema kwamba alikuwa asiye na elimu wala maarifa, lakini alifanywa kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu.

89 Akaanguka chini miguuni Pake. Alijua huyo alikuwa ni nani. Si kwamba tu alijua kuwa alikuwa ni nani, alimjua yule baba yake mkongwe mtauwa, ambaye ameshaondoka. Mnaona? Hiyo ilionyesha kwamba alikuwa ni Neno. Neno huyatambua mawazo yaliyoko moyoni mwao. Hilo ndilo hasa. Yesu aliwaangalia na akatambua mawazo yao. Mnaona? Na, hiyo, Biblia ilisema kwamba, "Neno la Mungu huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

90 Hiyo ilimfanya Neno, basi, yule Bwana-Nabii, yule Mungu-Nabii, zaidi ya nabii; Yeye, manabii wote walikuwa, pamoja na yote yaliyosalia ya Mungu. Mnaona? Yeye alikuwa Imanueli,

Mungu akiwakilishwa katika ukamilifu, katika Mwana Kristo Yesu. Sasa tunaona, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake.

91 Sasa, kama tukiangalia, basi Petro alishawishika kwamba yule baba yake mkongwe mtauwa alikuwa amemfundisha, na hii hapa ilikuwa ishara ya Kimaandiko kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

92 Huyo alikuwa ni Yeye jana, ni Yeye leo. Angewezaje kujitambulisha zaidi?

93 Sasa Yeye ni . . . Hakujitambulisha Mwenyewe kama daktari fulani mashuhuri, Ph.D., LL. Mnaona? Hakujitambulisha Mwenyewe kama kuhani fulani. Neno la Mungu lilimtambulisha. Neno likinena kupitia Yeye lilimtambulisha. Mnaona? Hivyo ndivyo walivyojua ni nini, kuwa Yeye alikuwa ni Nani.

94 Sasa kulikuwa na mmoja aliyesimama pale, jina lake Filipo. Naye Filipo alikuwa akifanya masomo ya Biblia, Maandiko, kwenye magombo, pamoja na jamaa aitwaye Nathanaeli. Basi alipoona hili likitokea, liliwasha moyo wake sana hata asingeweza kuvumilia tena. Alijua kitu Hicho kilikuwapo mahali pale. Yeye alikuwa ni Mtu wa kawaida tu, bali walijua kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

95 Kwa hiyo akakimbia kuzunguka kilima, ilikuwa yapata maili kumi na tano, kama ungepima mahali alipokuwa akihubiria, hapana shaka alienda siku moja na kurudi kesho yake. Naye akaenda kumtafuta jamaa huyu, aliyekuwa akisoma pamoja naye, katika Maandiko; mtu mwaminifu sana, mwenye haki. Mnao karibu hapa, watu wenye, wanaoweka maisha yao yote katika kulisoma Neno. Kwa hiyo alikuwa amesoma Neno. Ndipo Filipo akaenda kumwita, na labda alibisha mlangoni. Na—na—naye mke wa Nathanaeli akasema, "Mbona, alitembea tu kidogo kupitia shamba la mzeituni pale." Yeye ni mlimaji wa mizeituni.

96 Kwa hiyo akaenda, akakimbia huko kumwona, ndipo akamkuta amepiga magoti yake, chini ya mti mmoja, akiomba. Sasa Mkristo mwuungwana daima hutoa, huonyesha adabu, kwa hiyo a—alingojea mpaka akamaliza kuomba.

97 Akasema, "Njoo, umwone Yeye tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

98 Ndipo huyu Mwebrania, mwaminifu, jina lake Nathanaeli, akasema, "Sasa ngoja kidogo, Filipo. Hivi—hivi wewe umerukwa akili? Sasa hivi kungeweza . . . Ati ulisema wapi? Ulisema Jina la Mtu huyu ni nani?"

"Yesu wa Nazareti."

99 Akasema, "Sasa je! laweza jambo lolote jema kutoka Nazareti?"

100 Nami nafikiri Filipo alimpa jibu lililo bora kuliko yote mtu yeyote angeweza kumpa mwenzake. Alisema, “Njoo ujionee.”

101 Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, ujionee. Yachunguze Maandiko. Njoo ujionee!

102 Vema, labda, wakiwa njiani, akaanza kumwambia. Kasema, “Sasa, unajua, sisi tunajua. Tunajua, kutokana na Maandiko, kwamba Masihi huyu atakuwa ni nabii, maana Musa alisema alikuwa. Na Mtu huyu . . . Unamkumbuka maskini yule mvuvi aliyekuwa hawezi kutia sahihi jina lake kwenye risiti, wakati uliponunua samaki?”

“Naam.”

103 “Vema, Yeye alimwambia kuwa yeye ni nani.” Loo, ninamwazia Filipo akisema . . .

“Sasa ngoja kidogo,” ama, Nathanaeli, “Si—sina budi kuona hilo, kwanza.”

104 Wakati hatimaye alipofika mahali Yeye alipokuwa, alikuja pamoja na Filipo. Filipo alimleta kama tu vile mtu mwingine alikuleta, akaja katika Uwepo Wake, kwenye mkutano mahali Yesu alipokuwa akihubiri. Ndipo akamwangalia, Yeye alikuwa tu ni Mtu wa kawaida, amevalia kama mtu yeyote mwingine. Hakuonekana tofauti hata kidogo. Na Yeye daima hakupunguza mashambulizi. Daima alikuwa ni mtu aliyeweka mambo wazi.

105 Na wakati mwingine aliwazungumzia kwa mafumbo, hata wasiweze kuelewa hayo; hata na wanafunzi Wake. Hilo halikutatiza imani yao. Unaona, walimwamini.

106 Angalia, wakati mmoja, umati mkubwa ulikuwa umekusanyika kumzunguka, maelfu. “Alikuwa ni Jamaa mashuhuri! Loo, nabii huyu wa Galilaya, Jamaa mashuhuri!” Alienda kwa kila kanisa. Kila mtu alimhitaji. Lakini siku moja, alianza kuwahubiria fundisho, ndiposa hilo likabadilisha jambo hilo kidogo, mnaona. Hakuwa maarufu sana tangu hapo na kuendelea, mnaona. Bali ishara ilikuwa ikiambatana na Sauti.

107 Sasa tunaona, kwamba wakati Filipo alipokuja mahali Yeye alipokuwa, na yeye pamoja na Nathanaeli, Yesu aligeuka akamwangalia Nathanaeli, na kusema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

108 Sasa unasema, “Labda jinsi alivyovalia.” Wote walivalia sawa. Unaona?

“Halafu Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

109 Sasa hilo, karibu, lilimshtusha vibaya sana hakujua la kufanya. Akasema, “Rabi, ulinijua lini? Mbona, Wewe hujawahi kuniona. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza tumepata kukutana. Na wananiambia kuwa Wewe umekuwa ukiishi huko chini Bethania, na—na ulipataje—ulipataje kunijua?”

110 Vema, aliwazia, ajapo Masihi, kwamba—kwamba, "Mungu angechukua namna fulani ya mtambo na kuuvuta, na ushoroba wa Mbinguni ungeshuka chini kwenye . . . kwenye vipandio vyao vikubwa vya kimadhehebu huko nje, na kusema, 'Kayafa, ninamtuma Masihi wangu huko chini kwako sasa.' Atasema, 'Nimewasili.' Nao Malaika wangekuja, waseme, 'Huyu Ndiye.'"

111 Unaona, hiyo ndiyo sababu Yeye anafanya hivyo. Halafu inapita moja kwa moja juu yao hao watu, wanaolala, nao wasijue kilichotokea. Mnaona? Angalia, Huyo hapo. Alikuwa amesimama hapo.

Akasema, "Ulinijua lini, Rabi?"

112 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Loo, jamani! Ni macho ya jinsi gani!

113 Yeye anakuona sasa. Anakujua sasa. Ni yeye yule tu, jana, leo, na hata milele.

114 Ni macho ya jinsi gani! Maili kumi na tano, siku moja kabla, nyuma ya milima, "Nilikuona ulipokuwa chini ya mti."

115 Alifanya nini? Alikimbia akaanguka chini, na kusema, "Wewe ni . . . Rabi, Wewe ni Mfalme wa Israeli! Wewe ni Mwana wa Mungu!" Aliamini hilo. Kwa nini? Alitambulishwa kikamilifu kwamba Yeye alikuwa ni Neno. Kwa kuwa angeweza kutambua mawazo ya moyoni. Naam. Huyo hapo, amesimama pale.

116 Sasa kulikuwapo wale waliosimama pale, ambao hawakuamini hilo. La. Wengi wao hawakuliamini. Kulikuwako na baadhi ya makuhani na wengine wakisimama pale, walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli." Wao . . . Ja—ja—jambo hilo lilifanywa, Maandiko yalitambulishwa, na kisha ma—ma—makasisi wa siku hiyo ilibidi watoe jibu kwa kusanyiko lao. Na wasingeweza kulijibu kwa njia yo—yoyote nyingine, bali ama tu kusema kuwa Yeye ndiye au Yeye siye, kwa hiyo wakasema, "Mtu huyu hufanya haya kupitia Beelzebuli." Kwa maneno mengine, "Yeye ni mpiga ramli, roho chafu." Mtu yeyote anajua kwamba mpiga ramli ni shetani. Kwa hiyo akasema, "Mtu huyu hufanya uovu huu kupitia Beelzebuli."

117 Ndipo Yesu akasema, "Sasa, nitawasemehe kwa ajili ya hiyo." Dhabihu haikuwa imetolewa, upatanisho haukuwa umefanywa bado. "Lakini," akasema, "ajapo Roho Mtakatifu, kufanya hivyo, neno moja dhidi Yake halitasamehewa, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao." Kwa hiyo mnaona mahali inapotutupa leo.

118 Sasa, hili lilikuwa jambo kwelikweli, na, lakini Filipo na Nathanaeli waliamini kwa moyo wao wote. Sasa hivyo ndivyo Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe, jana, kuwa Masihi. Sasa, sote tunafahamu . . . Dakika chache tu sasa.

119 Sote tunajua kwamba kuna jamii tatu pekee za watu ulimwenguni, na hao ni wana wa Nuhu, Ham, Shem, na—na Yafethi; mnaona, na hao ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Sasa sisi, kama Wamataifa, tulikuwa makafiri, Warumi na chochote kile, katika siku hizo, Waanglo-Saxon, nasi tuliabudu sanamu. Lakini Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi. Nao Wasamaria walikuwa wakimtazamia Ma—Ma—Masihi.

120 Sasa, Yesu alisema, wakati alipokuwa njiani akielekea Yeriko, moja kwa moja chini ya kilima kutoka Yerusalemu, "Nina haja kupitia Samaria." Kwa hiyo akapanda kwenda huko, Samaria, na akaketi langoni, kwenye kisima. Kuna. . .Bado ungali tu kama ulivyokuwa. Hawajabadilika hata kidogo. Kuna mandhari ya kale kama haya hapa, nayo mizeituni imepandwa kwenye ukuta wa mawe. Ndipo—ndipo Yeye akaketi tu chini, na kuwatuma wanafunzi Wake katika mji huu mdogo, uitwao Sikari, kununua maakuli, chakula.

121 Basi walipokuwa wameenda, mwanamke mwenye sifa mbaya. . .Labda, kama nilivyosema, msichana huyo labda alisukumwa mtaani kutokana na, si utovu wa mtoto, labda utovu wa mzazi. Walimwacha kwenda nje mtaani, na labda ni msichana mwenye sura nzuri, naye alikuwa amefanya uovu.

122 Basi alikuja pale kuteka maji yake, kwa sababu asingeweza kuja na wanawali, wasingeninii. . .wanawake wazuri, wenye heshima. Wasingefanya hivyo. Wangeteka yao kwanza. Ndipo—ndipo hao wengine, makahaba na kadhalika, walikuja mchana. Wanawali waliteka yao. . .

123 Vema, jinsi nimewaona wakiweka mtungi wa galoni tano juu ya kichwa chao, ile nyungu kubwa, na moja juu ya kila bega, na kutembea moja kwa moja, wakiongea, kama wanawake wawezavyo, na wasimwage hata tone moja la hayo. Sijui wafanyavyo, bali hakika wao hulifanya.

124 Lakini wao, kupitia hapo, ndipo basi akaja kuteka maji yake kwa ajili ya siku hiyo. Hao wengine walikuwa wameenda; hapana shaka ilikuwa ni kwenye majira ya adhuhuri. Ndipo akachukua tambo na kuiweka kwenye winchi, kuitelemsha chini, kuchota ninii. . .

125 Mnaona, ni kama tu namna fulani ya nyungu. Na ni—nayo ina m—mkono ulioizunguka. Nao wakaweka misumari kama ndoana kwenye vishikizo, na, kwa kuwa ni nzito, ikifika chini, inapinduka. Kisha wanavuta maji juu. Jinsi tu ambavyo wakati mwingine tumefanya hapa katika nchi hizi, na kadhalika, lakini wana kitu kama kihori tunachotelemsha.

126 Sasa, tu—tunaona alianza kutelemsha mtungi huu kwenye kisima, ndipo akasikia mtu fulani, kasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Ndipo akaangalia kote, akaona Mwanaume mwenye umri wa makamo ameketi pale.

127 Lazima a—alionekana mwenye umri mkubwa kidogo kuliko aliokuwa nao, kwa sababu katika Yohana Mtakatifu 6 hapa tunaona, kwamba, wale waliokuwa kwenye karamu, walikuwa wakisema . . . Yeye alisema kile Yeye—kile alichokuwa. Nao wakasema, "Vema, Wewe wasema kuwa umemwona Ibrahimu, huku Wewe ni Mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini?" Mnaona, "asiyezidi," mnaona, hapana budi alionekana mwenye umri wa miaka hamsini wakati alikuwa tu na umri wa miaka thelathini. Kasema, "Wewe, Wewe hujapita umri wa miaka hamsini, nawe wasema umemwona Ibrahimu?"

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, Mimi niko." Mnaona?

128 Kwa hiyo basi tunaona kwamba hapana budi alionekana mwenye umri mkubwa kidogo, ameketi pale akiegemea upande wa ukuta.

129 Hatujui tu jinsi alivyoonekana. Nisingejua. Mtaalamu wa tiba ya magonjwa ya kiakili ama saikolojia anatuchorea picha, lakini ile ya Hofmann, na Sallman, na yeyote mwingine, lakini hayo ndiyo yale wanayowazia juu yake. Mnaona? Hatujui tu jinsi alivyoonekana.

130 Na pale Huyo alikuwa ameketi hapo, na ndipo akasema hivi. Na sasa Yeye akageuka, mwanamke akamgeukia, upesi, na kumjulisha, "Huu ni ubaguzi." Akasema . . . "Sasa hebu kidogo." Kasema, "Sasa, Wewe ni Myahudi, nami ni Msa- . . . mwanamke Msamaria, nasi hatuna mahusiano mmoja na mwenzake."

131 Ndipo kasema, Yeye akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji. Ninaleta, nikupe Maji usije kuchota."

132 Halafu, mazungumzo, alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake sasa, unaona, kuona ni nini kilichokuwa ndani yake. Sasa Baba alikuwa amemtuma huko juu, kama tu ninavyoamini Baba amenituma hapa. Mnaona? Lakini ni nini, sijui. Mnaona? Bali Yeye huyo hapo, Naye alikuwa akizungumza na huyo mwanamke.

133 Naye mwanamke akasema, "Loo, Wewe wasema, 'Kuabudu Yerusalemu.' Baba zetu waliabudu kwenye mlima huu," na kuhusu kisima, na kadhalika.

134 Akasema, "Wakati unakuja, na sasa upo, naye Mungu anawatafuta wale wanaoabudu katika Roho na Kweli."

135 Mazungumzo yakaendelea mpaka akagundua kilichokuwa shida ya mwanamke huyo. Ni wangapi katika kusanyiko langu usiku wa leo, wanaojua kilichokuwa shida yake? Hakika, alikuwa na waume wengi kupita kiasi. Kwa hiyo Yeye akasema . . . Akasema, "Nenda kamwite mumeo na mje hapa."

Ndipo akasema, "Sina mume yeyote."

136 Akasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye si wako."

137 Sasa angalia. Waangalie wale makuhani waliofunzwa, wakikosa kuliona hilo Neno likidhihirishwa. Alipofanya hayo mbele za hao makuhani, walisema, "Yeye ni Beelzebuli."

138 Mwangalie mwanamke huyu katika hali yake, hali aliyokuwamo, mwanamke mwenye sifa mbaya, alikuwa na waume sita, naye huyu hapa huko nje kisimani. Na mwanamke huyo katika hali hiyo, angalia, upesi alisema, "Bwana, naona kuwa Wewe ni nabii. Hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Naona kuwa Wewe ni nabii. Tunamtazamia Masihi, na, ajapo huyu Masihi, hii ndiyo ishara Yake. Atafanya haya ajapo." Amina. Loo, jamani!

139 Haya basi. Mwanamke huyo, katika hali yake, alijua mengi kuhusu Neno la Mungu kuliko nusu ya wahubiri nchini wanavyojua. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Alisema, "Ninajua, ajapo Masihi, aitwaye Kristo, ajapo, hayo ndiyo atakayofanya." Kama huyo alikuwa ni Yeye jana, huyo ni Yeye leo. Mnaona? Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe, kwa Myahudi na Msamaria pia. Mnaona? Angalieni, huyo alikuwa ni Yeye jana.

140 Akasema, "Ninajua, ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, lakini Wewe ni Nani?"

Akasema, "Mimi ndiye, ninayenena nawe."

141 Huyo akaenda mjini, akaacha mtungi huo wa maji. Kasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?"

142 Huo ulikuwa utambulisho Wake kwa Wayahudi Wake, na kwa Wasamaria; bali si kwa Mataifa, si wakati mmoja kwa Mtaifa. Lakini katika Luka, mlango wa 17, Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, wakati atakapokuwa akifunuliwa Mwana wa Adamu, kama ilivyokuwa hali iliyokuwa katika siku za Sodoma." Sasa, katika siku za Sodoma sasa. Basi tunafunga. Angalia, kulikuwa na . . .

143 Daima angalia, daima kuna matabaka matatu ya watu, kila mahali; moja ya hayo ni mwaminio, anayejifanya kuamini, na asiyeamini. Wako kila mahali. Angalia hilo.

144 Mwangalie Yesu akifananisha wakati wa Lutu na kuja Kwake. Sasa angalia, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu." Sasa, ni aina gani sasa? Alirejelea wakati huo. Alikuwa akikisoma kitabu kile kile cha Mwanzo tunachokisoma. Yesu alikisoma. "Siku za Nuhu," na, halafu, "kama siku za Lutu." Angalia nyuma na uone kile walichokuwa wakifanya katika siku za Nuhu, na katika siku za Lutu, maana ni Andiko lile lile.

145 Sasa tunaona, katika siku a Lutu, kulikuwako na mtu aliyekuwa ameitwa kutoka miongoni mwa watu. Naye alikuwa na kundi pamoja naye, ambalo linawakilisha Kanisa, la kiroho. Nalo Kanisa hilo, la kiroho, lilikuwa ni kundi la Ibrahimu.

146 Halafu alikuwa na mmoja humo ndani, mpwa wake, aliyemwacha, jina lake Lutu, na akaenda na kuishi Sodoma. Nazo dhambi za Sodoma zilihuzunisha nafsi yake; ila tu, mke wake asingemruhusu kufanya lolote juu yake. Alikuwa ni mshiriki wa vilabu vyote na kadhalika.

147 Na wapo Lutu wengi sana wanaoketi huku siku hizi, na wanajua kwamba kitu hicho ni kosa. Lakini mwanamke kanisa ambalo wanashiriki, iwapo wangesema lolote kulihusu, lingeichukua kadi yake; kwa hiyo hiyo ni tikiti ya mlo. Hivyo basi, tunaona kwamba hii . . .

148 Sasa ngojea. Ibrahimu alikuwa akimtazamia mwana aliyeahidiwa, (hiyo ni kweli?), wa kiroho, mwana aliyeahidiwa. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

149 Sasa, naye Lutu alikuwa huko chini, alikuwa amesahau habari za huyo mwana. Alikuwa tu huko chini akiishi na mke wake, na watoto wake, na wote huko chini Sodoma. Alikuwa meya wa mji, naye alikuwa ni jamaa mashuhuri. Mke wake alikuwa mwanachama wa vilabu vyote. Walikuwa wanaendelea vizuri sana.

150 Halafu basi angalia yale mazingira sasa. Sasa mnipe tu dakika moja au mbili zaidi, usikivu wenu, kwa makini. Angalia mazingira. Ulimwengu kamwe haujawahi kuwa katika hali hiyo, tangu, kama ulivyo sasa, mazingira hayo kikamilifu. Angalia hapa, kundi lililoitwa litoke. Sasa, kulikuwako na Malaika watatu waliomjia Ibrahimu, ndipo wawili kati yao wakateremka huko chini Sodoma. Mmoja wao alibaki na Ibrahimu, naye Yule aliyebaki na Ibrahimu . . .

151 Wale wawili waliteremka huko Sodoma na kuhubiri toba, na, "Ondokeni hapa! Ondokeni kwake," akasema.

152 Lakini Yule aliyebaki na Ibrahimu, angalia jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Ibrahimu. Sasa kumbukeni, Ibrahimu alikuwa "Abramu," siku moja ama mbili kabla ya hapo, naye Sara alikuwa—alikuwa si "Sara." Sasa yeye ni A-b-r-a-h-a-m, A-b-r-a-h-a-m, herufi saba. Naye mke ni S-a-r—r-a-h, tano, neema, unaona; sio S-a-r-r-a, bali S-a-r-a-h, unaona, Sarah. Basi mwangalie Huyu aliyeketi hapa sasa, akila ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na siagi, na kula ugali wa mahindi. Akiketi pale akila, huku akizungumza na Ibrahimu, ndipo akasema, "Ibrahimu." Alijuaje kwamba jina lake lilikuwa ni Ibrahimu? Neno. Yeye alikuwa Neno, alijua. "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sarah?"

153 Wanawake katika siku hizo hawakujiadhibisha kama wafanyavyo sasa, mwajua, ni sharti awe kwenye shughuli ya mumewe na kadhalika, mwajua. Walikaa mbali, mnaona, kwa hiyo wao . . . Kwa hiyo alikuwa katika . . . Akasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

154 Naye akasema, “Mimi,” sasa hicho ni kiwakilishi nafsi, sasa, “Nitakuzuru kulingana na ahadi.” Ilitolewa miaka ishirini na mitano kabla ya hapo. Mke ana umri wa miaka tisini, naye mume ana mia moja. Huyo hapo, kichwa chake chenye upara kinang’aa, masharafa yake meupe yananing’inia chini. Mke, maskini bikizee mkongwe akiwa na mkongojo kidogo mkononi mwake, huko nyuma, shali ndogo juu ya bega lake. “Nitakuzuru, nawe utamzaa huyo mtoto aliyeahidiwa.”

155 Angalieni, ndipo Sarah akacheka hilo. Akasema, “Mambo haya yangewezekanaje? Mimi ni mkongwe, na bwana wangu,” mume wake, “ni mkongwe, pia.” Mnaona ninachomaanisha, uhusiano wa kifamilia haukuwepo kwa miaka na miaka na miaka. Mbona, mke alikuwa na miaka tisini, naye mume alikuwa na mia moja. Tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa; mkondo wa maisha ya mume ulikuwa umenyauka na kufa. Hakuna shauku tena. Kasema, “Mimi, kama msichana mdogo, niwe na raha na mume wangu, yeye akiwa ni mkongwe pia?” Mbona, akacheka.

156 Naye Malaika huyo, au Mjumbe, Mtu huyo akiwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, kasema, “Kwa nini Sarah akasema hivyo?” Mnaona? Ilikuwa ni kitu gani? Sasa angalieni. Ndipo basi, baada ya dhabihu kutolewa, Yeye akatoweka.

157 Sasa kumbukeni, Ibrahimu alimwita Mtu huyo, “Elohimu.” Ni wasomaji wangapi wanaojua hilo? Mnalijua. Hiyo ni kweli. “Elohimu,” huyo ni Mungu Mwenyezi katika umbo la mwanadamu. Yeye alikuwa ni Neno, kwa kuwa angeweza kutambua mawazo. Mnaona?

158 Mungu katika mwili, inashuhudia nini? Kwamba, “Katika siku za mwisho,” Yesu alisema, “kabla tu… wakati anapofunuliwa Mwana wa Adamu kwa Kanisa Lake lililoahidiwa,” Kanisa ambalo haliko huko chini katika Babeli.

159 Tunalo kanisa la Babeli, mnajua hilo, madhehebu. Yako Babeli. Pia tunaye Bi—Billy Graham na Oral Roberts, na hao huko nje wakiwakemea kwa nguvu, pia. Tena kumbuka, yeyote wenu wanahistoria, hakujawahi kuwapo na mtu, katika historia yote ya nyakati za kanisa, ambaye amewahi kwenda huko Babeli, akihubiri, na jina lake linaishia na h-a-m, mpaka sasa: Billy G-r-a-h-a-m, ambazo ni sita, si saba. Huko angalia huyo mjumbe huko, akihubiri toba, na kuyapofusha macho yao kwa Injili.

160 Na kulikuwa na Mmoja kwa wale walioitwa watoke, Kanisa teule, lililokuwa likionyesha ishara ya kwamba Mungu alikuwa katika mwili.

161 Yesu alikuwa ni Mungu katika mwili. Na kama Yesu yuko ndani yako, usiku wa leo, bado ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika siku za mwisho, Mwana wa Adamu akijifunua Mwenyewe katika Kanisa Lake, mwili wa kibinadamu, akijitambulisha Mwenyewe. Mnalipata? Mnaona? Mungu, hapa chini katika Kanisa Lake, akijifanya Mwenyewe tena Neno,

Mwana wa Adamu akifunuliwa katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.

162 Sasa, kumbukeni, kama Mungu aliwapatia Wayahudi na Wasamaria ishara hiyo, kwamba Yeye alikuwa ni Neno, yule Nabii ambaye Musa alizungumzia, Wamataifa . . . Baada ya wao kuwa na miaka elfu nne ya kumtazamia, sisi tumekuwa na miaka elfu mbili ya kumtazamia, Yeye hana budi kujitambulisha Mwenyewe kwa njia ile ile kwetu, kama alivyofanya wakati ule, la sivyo Yeye alikosea wakati alipojitambulisha wakati ule. Mungu hana budi kutenda wakati ule ule, kwa njia ile ile kila wakati, la sivyo alikosea wakati wa kwanza. Kama alimwokoa mwanadamu juu ya msingi wa imani yake . . .

163 Angalieni, Mungu kamwe habadiliki, enyi marafiki. Wakati mwanadamu alipotea, katika bustani ya Edeni, naye alikuwa akitafuta rehema, Mungu alifanya uamuzi jinsi angemwokoa mwanadamu. Naye alimwokoa kwa damu iliyomwagika ya asiye na hatia. Hiyo ni kweli? Kamwe Yeye hajabadilisha hiyo. Tumejenga miji, minara; tumejenga madhehebu, mifumo ya elimu, na ingali inabaki vile vile; tunayo madhehebu na kila namna ya mambo. Lakini Yeye huokoa tu kwa Damu. Hawezi kuibadilisha. Mungu daima hubaki mwaminifu kwa mpango Wake, Neno Lake. Chochote alichofanya kwa mara ya kwanza, hana budi kukifanya tena, la sivyo alikosea hapo kwanza.

164 Hivyo basi, chochote Neno hili la Mungu linachoahidi, hicho ndicho hakina budi kuwa. Naye Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hana budi kufanya vile vile. Hana budi kufanya vile vile. Hana budi kuwa ni yeye yule, kama alivyoahidi katika siku za mwisho kuwa angekuwa katika Kanisa Lake.

165 Pia, kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho Kanisa liliyopata kabla ya mwana aliyeahidiwa kuja. Ibrahimu alikuwa ameona ishara nyingi na maajabu, lakini hiyo ilikuwa ndiyo ya mwisho, kuzuriwa kwa mwisho kabla mwana aliyeahidiwa kuja. Je! hiyo ni kweli? Tafuta kujua.

166 Sasa, kanisa, angalieni, kama ilivyokuwa katika siku hiyo. Tumekuwa na kila namna za ishara, uponyaji, miujiza, kunena kwa lugha, utabiri; bali, kumbukeni, hatuna budi kuwa na ishara ya mwisho kabla tu . . . Kumbukeni, huo ulikuwa ni ulimwengu wa Mataifa ulioteketezwa. Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati huu. Kabla tu ya moto, Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe. Ah, sikia, "Bado kitambo kidogo, ulimwengu hautaniona tena, bali hata hivyo ninyi mtaniona wakati wa mwisho. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, mwisho wa ulimwengu." Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

167 Baba yetu wa Mbinguni, tunaambiwa katika Maandiko kwamba Mungu alimfufua siku ya tatu. Tunaambiwa katika

Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, kifungu cha 12, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi naye atazifanya pia. Hata nyingi zaidi atafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu."

168 Bwana Yesu, saa zinazidi kuingia giza na nuru kufifia. Kanisa limepotea, nje nyikani, linatangatanga huku na huku, kuanzia watu wakienda kutoka shirika moja hadi lingine, kutoka dhehebu moja hadi lingine.

169 Njoo, katika Neno Lako lililoahidiwa. Njoo, Bwana Yesu, na uingie ndani yetu, usiku wa leo. Ingia ndani ya kila moyo uliopo hapa. Ingia ndani ya moyo wangu na maisha yangu. Na ninaomba Wewe ujitambulishe Mwenyewe pamoja na imani yetu Kwako, usiku wa leo, kwamba umefufuka kutoka kwa wafu. Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jalia tukuone Wewe, Bwana, katika kundi hili dogo la watu maskini. Kama tulivyokusanyika hapa sote, tupo hapa nje kwa sababu tunatafuta Uzima. Ni jambo kuu jinsi gani, kujua kwamba ufufuo na Uzima yuko miongoni mwetu, akijitambulisha Mwenyewe, si kwa jambo fulani la kiini macho, bali kulingana na Neno lililoahidiwa. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na kama siku za Lutu, wakati anapofunuliwa Mwana wa Adamu."

170 Ninaomba, Baba, kwamba Wewe utatujalia, usiku wa leo, kwamba, watu hapa walio wagonjwa na wahitaji. Na wale walio wagonjwa katika nafsi, wale ambao wamejiunga tu na kanisa na hawajui chochote kuhusu kumpokea Roho Mtakatifu, na kumwona Huyo akiitikia kila Neno kwa "amina," lililo kwenye Biblia. Biblia ni kitabu cha mafumbo kwao; hawawezi kuielewa. Jalia wampokee Mfasiri wa Neno, usiku wa leo, asiyehitaji mtu yeyote kufasiri Hilo ila Yeye, akilifanya kuwa halisi kwa maisha yao. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

171 Huenda nikapitisha dakika kumi, usiku wa leo, kwa kuzungumza kirefu. Samahani. Bali tunaenda tu kuita kadi chache za maombi, na wapate kuwaombea.

172 Sasa nitawaulizeni jambo moja, sasa, msi—msisimame na kuzungukazunguka. Mtafanya hivyo? Kaeni tu kwa utulivu. Isipokuwa, uwe tu—kitu fulani tu, kama vile mtoto mchanga ama kitu fulani, inakubidi kukichukua. Lakini kama mtaketi tu kwa utulivu kwa dakika chache, ninii tu . . .

173 Na hebu tuone kama Yeye atakuja, kama atakuja na kujitambulisha Mwenyewe, usiku wa leo. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Nawe waweza kuona Uhai Wake ukiishi, kweli, ukitenda kile Yeye alichotenda wakati ule, kwani ingembidi kutenda kile kile. Mnaona?

174 Akasema, "Mimi ndimi . . ." Kitu gani? Mzabibu. "Nyinyi ni . . ." Kitu gani? Matawi. Vema, sasa, ni kwa njia gani . . . Aina

ile ile ya Uhai ulioko ndani ya Mzabibu itabidi uwe katika tawi. Sasa angalia, unasema, humu ndani leo . . .

175 Enyi watu, si nyote ni wakulima wa tunda hapa, machungwa na kadhalika? [Mtu fulani anasema, "Plamu."—Mh.] Nini? ["Plamu."] Plamu. Vema. Mnalima . . .

176 Angalieni hapa. Ikiwa mzabibu wako umezaa na kutoa tawi kutoka kwenye mzabibu huo, na tunda lolote lile lililoko kwenye mzabibu huo, mzabibu huo ukizaa tawi jingine, kitakuwa ni kitu kile kile.

177 Nilikuwa nimesimama na rafiki yangu, miaka kadhaa iliyopita, huko Arizona, Bw. Sharrit. Naye alikuwa na mchungwa pale, nafikiri ulikuwa na matunda tisa mbali mbali juu yake. Nao ulikuwa na limau, balungi, chenza, kangaja, chungwa. Nikasema, "Ni mti wa aina gani huo?"

Kasema, "Ni mchungwa."

"Vema," nikasema, "vema, hayo yaliingiaje humo?"

Akasema, "Niliipandikiza."

178 "Loo," nikasema, "nimeona, Ndugu Sharrit." Nikasema . . . Nafikiri Ndugu Sharrit alikuwa pamoja nami wakati wa mwisho nilipokuwa hapa. Basi kwa hiyo nikasema, "Vema, Ndugu Sharrit, sasa, mwaka ujao, yote yatakuwa ni machungwa, na hayatakuwa . . . "

179 "Loo, la. La, la. A-ha." Akasema, "Mbalungi utazaa balungi. Mlimau utazaa limau."

"Vema," nikasema, "vipi hiyo?"

Akasema, "Yote ni aina ya mchungwa."

180 "Loo!" Nikaelewa basi. Nikasema, "Jambo ndilo hilo." Nikasema, "Asante, Bwana."

181 Mnaona, tunapandikiza madhehebu yetu kwenye Mzabibu huu, yataishi kwa Mzabibu, bali linazaa tunda la aina yake. Bali mti huo wa mchungwa ukiwahi kuzaa tawi jingine, litazaa machungwa. Na kama Uhai huo ulitoka kwa Yesu Kristo, nao waliandika Kitabu cha Matendo nyuma ya Kanisa lile la kwanza, kama likizaa jingine, litaandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake, kwa kitu kile kile, kwani halina budi kuwa ni lile lile. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

182 Hatuna wakati wa kuyaleta yote. Kwa hiyo hebu tu, upesi sasa, wakati tukiwa tu na dakika chache, tuanzie kwenye M moja, mbili, tatu, nne, tano. Inueni mikono yenu, nyinyi mlio na . . .

183 Ni nani aliye na M moja? Je! ipo? Kadi ya maombi M moja? Mna hakika . . . Loo, M moja, unayo kadi ya maombi namba moja? Ni nani aliyekuwa nayo? Mama yule pale aliye na namba moja, njoo moja kwa moja hapa. Hiyo ni—je! hapa ndipo mnapozileta? Namba moja, njoo hapa, mama.

184 Namba mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? Papa hapa. Vema, njoo moja kwa moja hapa, bwana. Tatu, inua mkono wako.

185 Sasa waangalie watu hawa kwenye machela, wakati kadi zao zikiitwa, wabebeni muwalete hapa juu, maana sidhani yeyote kati yao anaweza kutembea, na yule mwanamume pale kwenye kiti cha magurudumu. Vema.

186 Moja, mbili, tatu. Kadi ya maombi namba tatu? Vema, tatu. Nne, nne, kadi ya maombi namba nne. Hebu. . . Iangalie kadi yako sasa, upesi sana. Tano. Pale pale, simama. Nenda moja kwa moja hapa, bwana. Sita, kadi ya maombi namba sita, sita. Saba. Ni—ni . . . Watu hawa huzungumza Kifaransa? Ama, saba, vema. Nane, nane. Angalieni, huenda ni mtu fulani aliye kiziwi, au kitu kama hicho. Nane, vema. Vema, sasa nyinyi angalieni. Angalieni, mabawabu waangalie kadi moja kwa moja hapo. Nane, tisa; tisa, kumi. Huwezi kujua mahali walipo. Zinachanganyishwa tu na kutolewa kila mahali, mnaona. Kumi. Vema. Kumi na moja, kumi na moja. Unayo kumi na moja, kadi ya maombi namba kumi na moja? Vema, hapa, kumi na moja.

187 Kumi na mbili, kadi ya maombi namba kumi na mbili. Je! inaweze-. . . Wanazungumza Kifaransa? [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ati nini, nini, aha? Loo. Ikiwa nimekutana na wewe . . . Wewe huzungumza Kifaransa, sivyo, . . .? . . . Kumi na mbili.

188 Kumi na tatu. Angalieni, huenda ni mtu fulani aliye kiziwi, mnaona; hawawezi kusikia, wameketi tu hapo, wameshika kadi. Kumi na tatu. Kumi na nne, kumi na nne, kadi ya maombi namba nne-. . . kumi na nne, kumi na nne. Angalieni baadhi, mwangalie jirani yako, huenda ameshika kadi, ameketi hapo kiziwi, mwajua, naye hawezi kusikia chochote, basi sisi . . . inaenda upogo namna hiyo. Kumi na nne. Sasa, kadi za maombi hazibadilishanwi, na hayana budi kuwa; mtu hana budi kuja achukue kadi yake na kushikilia kadi yao. Labda mtu alitoka.

189 Vema, kumi na tano. Vema, hebu, tutasimama. Vema, endelea. Unayo kumi na tano, endelea. Hiyo ni sawa.

190 Sasa hebu tungoje moja kwa moja hapa kidogo tu, basi, mnaona, huku tukijiweka tayari. Vema, sasa, tafadhali iweni na kicho kabisa na mketi kwa utulivu, kwa muda mfupi tu.

191 Sasa, yote niliyosema usiku wa leo, ni wangapi wanaamini ni ahadi ya Maandiko. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Sasa, sasa, je! ni kweli, ndilo jambo linalofuata. Mnaona? Je! ni kweli? ["Amina."] Vema, ikiwa ni kweli, basi ni Neno la Mungu, basi Yeye anawajibika kwa Neno Lake, ahadi yoyote. Je! mnaamini hilo? ["Amina."] Sasa iwapo atajitambulisha Mwenyewe kwa njia ile ile aliyojitambulishia Mwenyewe kwa Myahudi na Msamaria pia, na akasema Yeye atafanya hivyo tena katika siku za mwisho kwa Mataifa,

je! mtaamini? Inua mkono wako, useme, "Nitaamini hilo." ["Nitaamini hilo. Amina."] Sasa kunao sasa . . .

192 Watu hawa hapa, si—sidhani kuna yeyote hapa anijuaye. Ni—nilifikiri niliona mtu fulani hapa muda mfupi uliopita, niliyemjua, bali na—nafikiri wameondoka, mtu fulani. Kila mtu ni mgeni . . . Ni wangapi huko nje wanaojua kwamba sijui lolote kukuhusu? Inueni mikono yenu, popote, kwenye roshani, popote ulipo. Hakika. Sasa angalia, wakati wakiwaandaa huko chini.

193 Kulikuwako na maskini mwanamke fulani wakati mmoja, na hebu tuseme hakuwa na kadi ya maombi. Alikuwa na kitu fulani bora. Alikuwa na imani, naye akasema, "Ninamwamini Mtu huyu. Kama ninaweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitakuwa mzima." Ni wangapi wanajua hayo ni Maandiko; yule mwanamke mwenye ninii ya damu . . .? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

194 Sasa hebu tuangalie sasa, hili, Andiko jingine, wakati, hadi watakaponiambia kuwa wako tayari.

195 Mwanamke huyu hakuwa na kadi ya maombi, bali alikuwa na imani. Akasema . . . Hakuwa na Andiko kwa hilo, kama ulivyo nalo, usiku wa leo. Lakini, hakuwa na Andiko, bali alisema, "Kama ninaweza kugusa vazi Lake! Ninamwamini Mtu huyu. Nitaponywa." Ndipo akajipenyeza katikati ya umati, na kuligusa vazi Lake.

196 Sasa, hivi mliwahi kuona vazi la Kipalestina? Linapwaya, na pia lina vazi la ndani. Sasa, kama uligusa mfu- . . . mfuko wangu wa koti langu, nisingehisi huo. Unaona? Nalo vazi Lake lilipwaya mbali *hivyo* kutoka Kwake.

197 Hakuhisi mguso wa kimwili. Kwa hiyo, hata alithibitisha hilo, alisema, "Ni nani aliyenigusa?"

198 Naye Petro akasema, "Mbona, Bwana," kwa maneno mengine, "Utafanya watu wafikirie Wewe ni—Wewe una kichaa. Unaona, usi—usi—usiseme hivyo. Unaona? Usifanye hivyo, maana kila mtu anakugusa."

199 Akasema, "Bali ninatambua kwamba nimedhoofika." Nguvu zilimtoka. Huo ni uweza. "Nimedhoofika." Ndipo akaangalia kote kwenye umati, na akampata mwanamke huyo, akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na kusema imani yake ilikuwa imemponya. Ni wangapi wanajua hadithi hiyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni kweli.

200 Sasa, sasa wahudumu, ndugu hapa juu. Sasa, Biblia ilisema, kwamba, "Yeye ndiye kuhani Mkuu usiku wa leo awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.]

201 Ni wangapi huko nje wanaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

202 "Yeye ni nanii Mkuu. . . aliyeketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, usiku wa leo, Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Basi Yeye angefanyaje kama ungemgusa? Angefanya vile vile alivyofanya wakati ule, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

203 Kwa hiyo, sasa, wewe amini, na uombe, na uamini, uone yale Mungu afanyayo. Uone kama unaweza kugusa vazi Lake. Wewe mguse, useme, "Bwana Yesu, ninajua huyo mhubiri hanijui. Hakujua chochote kunihusu, bali Wewe wajua. Kwa hiyo, Bwana, ninapokugusa Wewe, Wewe nena kupitia yeye." Sasa ni kitu gani hiki?

204 Karama si kitu unachochukua kama mu—mundu, ama ki—ama kisu, na kupenya kwa kisu hicho kama karama, ukikata, hiyo si karama ya Mungu. Karama ya Mungu ni. . . Karama ya Mungu ni kujua jinsi ya kujiachilia, kujiondoa njiani, kusudi Mungu aingie na akutumie. Si kitu fulani ulicho nacho mkononi mwako, unachoenda ukichoma kwacho. Unajiondoa tu njiani, na kumwacha Roho Mtakatifu akutumie. Sasa, sasa, je! si hivyo ndivyo ambavyo nyinyi watu hufanya mnaponena kwa lugha, enyi Wapentekoste? Jiondoe tu njiani.

205 Vema, hicho ndicho kitu kile kile hapa sasa. Na kama atatujalia, je! mtaliamini na kulikubali, kujua kwamba Uwepo Wake upo hapa? Hamtahitaji kadi yoyote ya maombi wakati huo.

206 Vipi kuhusu Ha—Hakimu wa Mbingu na nchi, kama vile Ibrahimu alivyomwita, "Hakimu wa Mbingu na nchi, hivi Wewe ungekosea?" Unaona? Kama Yeye, katika siku hizi za mwisho, kulingana na ahadi Yake sasa. . . Kote katika juma, tutaendelea tu kurusha Maandiko humo, kuwaonyesha kwamba hilo ni Kweli. Na kama Yeye yupo hapa pamoja nasi, usiku wa leo, dhahiri sana hata unaweza kuona kazi Zake na kujua Yeye yupo hapa, kama Neno Lake lililoahidiwa; si kitu fulani cha kubuni, bali kile Neno Lake lilichoahidi angekuwa; basi wewe mwamini.

207 Sasa, sijui sasa. Wakati mwingine, maono yakija, basi yataninii. . . sijui ninachosema; kwa hiyo acha ma—maikrofoni, na chochote kile, yeyote anayeidhibiti, aiongezee sauti. Ninawatakeni kuwa na kicho kabisa kwa muda mfupi.

208 Sasa huyu ndiye yu—yule mama? Sasa, hapa, imetokea kuwa ni mwanamke, kile tu nilichokuwa nikuzungumzia, Yohana Mtakatifu 4, mwanamke na mwanamume wanakutana kwa mara ya kwanza maishani. Mimi ni mgeni kabisa, na hatufahamiani kabisa mmoja na mwenzake. Ikiwa hiyo ni kweli, ili tu uinue mkono wako, acha watu waone (Mnaona?) hatujawahi kukutana maishani. Huyo hapo amesimama mwanamke huyo, mimi hapa, kitu kikamilifu tu cha ninii yetu. . . Wewe siwe yule mwanamke pale, nami siye Bwana, bali ni—ni watu wawili wanaokutana

hapa, mahali padogo tu kama walipokutana, mara ya kwanza maishani. Sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, labda Yeye angezungumza nawe dakika moja, unaona, kama alivyomfanyia yule mwanamke. Unaona? Sasa, Baba . . .

209 Siku ile nyingine, wakati, hivi majuzi ambapo Ndugu Borders hapa alikuwa, tulikuwa na mialiko mia sita na kitu hapa Marekani, mbali na nchi za ng'ambo. Akasema, "Baton Rouge, Louisiana, lipo kundi la watu huko chini."

210 Nikasema, "Endelea, hiyo ni sawa, anzisha mkutano huko chini." Nilijihisi kufanya hivyo. Mimi hapa. Sasa sijui kinachofuata. Nipo tu hapa. Hayo ndiyo yote nijuayo. Mnaona?

211 Sasa wewe hapa, mtu. Ninahubiri Neno, nikisema kwamba, "Yeye hajafa. Yu hai." Yu hai, na ameahidi kujitambulisha Mwenyewe katika miili yetu, mwili wa kibinadamu, kama alivyofanya huko nyuma. Mnaona? Yote aliyokuwa Mungu, alimimina ndani ya Kristo; yote aliyokuwa Kristo, alimimina ndani ya Kanisa. Huyo ni Yeye, Kristo ndani yetu. Sasa kama Bwana Yesu amefufuka kutoka kwa wafu . . .

212 Nami nitakuleta hapa juu na kukuwekea mikono, na labda kama baadhi ya ndugu zetu wainjilisti, ambalo ni kweli kabisa, na kuweka mikono juu yako, kusema, "Udhaifu wako umetoweka. Bwana amekuponya." Hiyo ingekuwa sawa. Unaweza kwenda. Hilo ni sawa. Hakika ninaidhinisha hilo, asilimia mia moja. Hilo ndilo Biblia ilisema.

213 Lakini sasa vipi kama Yeye akisimama hapa na kukuambia jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani ambalo hukupaswa kufanya? Kama anajua kile ambacho umekuwa, na kukuambia kile umekuwa, nawe unajua kama ni kweli ama si kweli, basi Yeye akikuambia kile siku zako za usoni zitakavyokuwa; kama hiyo ni kweli, hii itakuwa kweli, pia. Je! hiyo ni kweli? Hiyo itaifanya kuwa ni Yeye, unaona. Sasa ninasema tu hayo ili kuwasiliana na roho yako. Unaona, kama tu Yeye alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, "Niletee maji ninywe."

214 Sasa kuna jambo moja ninalotaka uone sasa. Mwangalie huyu mwanamke, angalia kubadilika kwa kuonekana kwa uso wake, sasa hivi. Unaona? Anafahamu kwamba jambo fulani linaendelea. Ni wangapi waliowahi kuona picha ya hiyo Nuru? Mnaona, Ipo moja kwa moja juu ya mwanamke huyo sasa, mnaona. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Mnaona, Hiyo ni . . . Mnaona Hiyo hapo? Ni namna ya Nuru ya kaharabu, ikisonga. Sasa tatizo lake ni hili . . .

215 Sasa kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, lakini siwezi. Siwezi kukuponya. Mungu ndiye mponyaji; imani yako kwa Mungu.

216 Wewe una wasiwasi kupindukia. Unasumbuliwa na hali ya wasiwasi, na tena una shida fulani katika koo lako.

Unazungumza kwa shida, ni mnong'ono tu. Ni tezi ya kikoromeo. Hiyo ni kweli. Sasa je! unaamini? Sasa hebu kidogo, ili tu wasifikirie nilikuwa nikibahatisha hayo, hebu kidogo tu, mnaona. Mimi, naam, ninasema hayo ili watu wasifikirie... Wewe ni mtu mzuri, nami nina uhusiano mzuri na Roho Mtakatifu, pamoja na wewe, unaona. Kwa hiyo, sasa, naam, umeshauriwa kufanyiwa upasuaji, lakini ulikataa. Hiyo ni kweli kabisa. Unamtarajia Mungu... Naam, bwana.

217 Kitu kingine, una ugonjwa wa pumu unaokusumbua. Hiyo ni kweli. Sivyo? Sasa, unaona, Kitu fulani hapa kinakujua. Hiyo si ni kweli? Je! unaamini ni Yeye? Basi amini hilo, na uondoke mimbarani, ukaponywe. Basi amini kwa moyo wako wote. Amina. Je! unaamini sasa kwa moyo wako wote? "Kama unaweza kuamini!"

218 U hali gani, bwana? Mimi ni mgeni kwako, nadhani. Ikiwa sisi... [Ndugu huyo anasema, "Nilikutana nawe mara moja hapo kabla, Baton Rouge."—Mh.] Wewe, wewe ulikutana nami nilipokuwa hapa hapo kabla, Baton Rouge. Jamani, hiyo imekuwa ni muda mrefu uliopita, sivyo? Nadhani imekuwa miaka kumi na miwili, au zaidi, labda zaidi, na labda ni miaka kumi na minne. Vema, nisingejua ni nini, chochote kukuhusu, si zaidi ya vile ulikuwa kwenye mkutano, ama kitu fulani, bali Mungu anakujua.

219 Nayo ni Nuru. Inanibidi kuangalia Hiyo, kuona mahali inapoenda, unaona, kwa watu wengine. Hiyo, ni upako. Sasa ikiwa Bwana Yesu ataninii... Sisi hapa tuna... Ni—ninaamini mtu wa mwisho alikuwa m—mwanamke. Sasa ni kama tu ndoto, unaona, uliota kitu fulani.

220 Sasa, sasa wewe ni mwanaume. Na sasa wakati Yesu alipokutana na mwanaume, Simoni Petro, wakati Yeye alipojitambulisha Mwenyewe. Jina lake lilikuwa ni Simoni, wakati huo. Yeye akamwita Petro. Akasema jina lake lingekuwa, baada ya hapo, ataitwa Petro. Kama Bwana Yesu ataniambia kilicho shida yako, je! utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, na kuamini kwamba Yeye yupo?

221 Je! kila mtu humu ndani ataamini jambo lilo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Labda unajulikana hapa, kwa sababu umetoka mjini.

222 Ninaona kitu fulani, kana kwamba umefadhaishwa na jambo fulani. Hiyo ni, naam, ndivyo ilivyo, maana ni damu, shida fulani kuhusu damu. Unatokwa damu katika matumbo. [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo hufanya vidonda humo, pia. Unaona? Sasa, hiyo ni kweli, sivyo? ["Amina."]

Sasa mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

223 Hivyo ndivyo Bwana wetu angelifanya. Sivyo? Huyo ni Yeye akifanya hilo. Hivi huamini hilo? [Ndugu huyo anasema,

"Amina."—Mh.] Vipi kama . . . Yesu alimwambia Simoni jina lake. Vipi kama Mungu angeniambia jina lako, je! ungeniamini? ["Amina."] Vema, bwana. Lewis Carrie. ["Amina."] Hiyo ni kweli kabisa. Nenda zako. Amina. Uwe na imani katika Mungu.

224 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

225 Sasa mimi ni mgeni kwako, dada. Sikujui, sijawahi kukuona, maishani mwangu. Wewe ni mwanamke tu aliyesimama hapa. Mdogo wa umri kuniliko mimi, tulizaliwa umbali wa maili nyingi, na kuachana kwa miaka. Lakini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Je! unaamini hilo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unaamini hi—hiyo?

226 Sasa, unajua, ukisimama kando ya mwanamume, ndugu yako hapa, isingekufanya kujisikia namna hiyo. Unajua hapana budi kuwepo na kitu kingine, katika Uwepo huo, mtamu kabisa, mpole, mnyenyekevu. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, kusudi kusanyiko lijue, inua tu mkono wako ili waweze kuona. Mnaona, ninamwangalia moja kwa moja, hiyo Nuru ikimzunguka.

227 Mama huyo amesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hayupo hapa kwa ajili yake mwenyewe. Ni kwa ajili ya binti yake. Hiyo ni kweli. Unaamini Bwana anaweza kuniambia kilicho . . . Unapanga kumleta msichana huyo kwenye mkutano. Lakini wewe—wewe unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yake? Je! utaamini na kuweka leso hiyo juu yake, na kuamini kwamba ataponywa? Iko mgongoni mwake. Hiyo ni kweli. Hiyo ni hakika. Nenda, amini sasa. Iweke hiyo juu yake, atapona. Vema, amini tu.

228 Je! unaamini kwa moyo wako wote? "Kama unaweza kuamini! Mambo yote yanawezekana kwao waaminio."

229 U hali gani? Hatufahamiani, nadhani. Sikujui, hunijui, bali Bwana anatujua sote wawili, kwa hiyo tukiwa ni mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza. Sasa, Bwana wetu alisema jambo lile moja kwa mwanamke yule, na mji wote ukaamini. Hawakuninii . . . Hakufanya hivyo tena. Alilifanya tu mara moja, na mji wote ukaamini.

230 Sasa usi—usiogope. Hakuna kitu kitakachokusumbua. Itakusaidia, unaona, maana sidhani wewe ni mkosoaji, ama wewe . . . mtetemo wa kile . . . Roho wa Bwana asingekuwa akija namna hiyo. Wewe ni mwaminio, kwa hiyo huna haja ya kushtushwa kuhusu chochote.

231 Unaugua he—henia. Hiyo ni kweli kabisa. Na je! unaamini kwamba Bwana Yesu atakuponya huo? Vipi kama ningekuambia jambo jingine lililo shida yako, lingekutia nguvu kuamini? Una kifundo. Kama ninaweza kukuambia . . . Hakiko kwenye shavu lako. Kiko mgongoni mwako. Kama hiyo ni kweli, punga mkono. Vema, sasa amini. Nenda, amini vyema, na uponywe.

232 Je! mnaamini sasa, kila mmoja wenu, kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa hiyo yapaswa kumfanya kila mtu kutambua kwamba uko katika Uwepo wa Mungu. Vema.

233 Bwana, unaamini Mungu anaweza kuuponya huo ugonjwa wa baridi yabisi na kukufanya mzima? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Kama unaamini, endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana Yesu."

234 Sasa njoo huku, mama. Ninakuona ukijaribu kuamka kutoka kwenye kitanda, pia, pole pole sana, baridi yabisi, pia. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakufanya mzima. Unaamini hilo? Vema, endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana Yesu. Hakika ninaamini hilo, kwa moyo wangu wote." Vema.

235 Njoo, bwana. Hali ya wasiwasi, na kadhalika, na tezi dume. Na, baridi yabisi, pia; na kuweka hiyo juu yake, amini kwa moyo wako wote. Uwe mzima, pia. Sasa endelea tu kutembea, ukimwamini Mungu. Na itakuwa sawa, kama tu unaweza kuamini. Vema.

236 Njoo upande huu, mama. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya tatizo hilo la moyo ulilo nalo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema, endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana. Nakushukuru kwa kuniponya tatizo la moyo wangu." Vema.

237 Njoo, bwana. Je! unaamini yale unayoona kuwa ni Kweli? Vipi kama nikikwambia tatizo hilo la tumbo liliponywa, pale chini, na uende ule chakula chako cha jioni, je! utaamini? Vema. Nenda, ukale chakula chako cha jioni, utakuwa mzima.

238 Huna budi . . . Umetiwa uvuli; kansa. Je! unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima, na kukuponya? Vema, endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana Yesu. Ninaamini kwa moyo wangu wote."

239 Pia, moyo wenye wasiwasi. Je! unaamini kwamba Mungu atauponya na kuufanya mzima? Endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana Yesu," na uamini kwa moyo wako wote.

240 Njoo upande huu, mama. Angalia hapa. Kitu chako kuu . . . Unayo mambo mengi kasoro kwako, shida ya kina mama. Bali shida yako kuu ni tatizo la moyo linalokusumbua vibaya sana. Je! unaamini kwamba Mungu atauponya na kukufanya mzima? Zidi tu kusonga mbele, ukisema, "Asante, Bwana Yesu. Ninaamini kwa moyo wangu wote." Vema.

241 Njoo, bwana. Unayo mambo mawili au matatu yaliyo shida kwako, matatizo. Bali jambo lako kuu unalotaka niombee, ama kuomba kulihusu, ni hiyo baridi yabisi uliyo nayo. Iangalie

baridi yabisi. . . Zidi tu kusonga, ukiamini, na haitakubidi kuichukua fimbo hiyo. Amina. Amini kwa moyo wako wote.

242 Unalo tatizo la tumbo. Limesababishwa, limekuwa nawe kwa muda mrefu, ni hali ya wasiwasi inayofanya tumbo kuwa na vidonda. Ukinywa chochote, ambacho ni—ambacho kwa namna fulani ni kama kahawa au kitu kingine, huchachuka kinywani mwako na mambo kama hayo. Nenda, amini sasa, nalo halitakusumbua tena. Yesu Kristo atakufanya mzima.

243 Njoo, mama. Je! unaamini kwamba Yesu Kristo. . . Hebu kidogo tu. Hebu kidogo tu.

244 Je! unaamini kwamba Mungu anaponya hayo mapindi, unayeketi hapo, na kukuponya kutokana na hayo mapindi? Je! unaamini hilo, kwa moyo wako wote? Mama huyo anayeketi hapo amevaa gauni linaloonekana lenye mirabamiraba. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya na kukufanya mzima? Ulikuwa na imani nyingi kuliko ulivyodhania ulikuwa nayo. Ni sawa. Umekwisha sasa. Wewe amini.

245 Unawazia nini? Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya na kukufanya mzima kutokana na hali hiyo ya wasiwasi, unayeketi hapo, huyo mwanamume? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Unaamini, je! unaamini hilo? Sasa ni Nani uliyemgusa? Kamwe hakunigusa mimi. Ulimgusa Yeye. Hilo ndilo lilifanya hilo. Amina.

246 Ulianguka kwenye paja lako, na ulikuwa na tatizo la jicho. Macho yako yanaharibika sana hata ni vigumu kwako kutembea. Je! unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? Amini hilo, nawe unaweza kuupokea. Amina. Nakupa changamoto kuliamini.

247 Tatizo, tatizo la tumbo, ndio kwanza likuache. Je! unaamini? Sasa nenda zako na ushangilie, na kusema, "Asante, Bwana," upate afya.

248 Maskini mama huyu anayeketi papa hapa, amevaa gauni linaloonekana la kijani kibichi. Unajaribu kugusa kitu fulani. Unaomba. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kile unachoombea? Aliondoe tatizo hilo la kibofu nyongo, na unafikiri utakuwa mzima? Huyo mama, kidogo ni mnene hapo, amevaa gauni, kubwa. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya tatizo hilo la kibofu nyongo, kama ungeweza kuamini? Mungu atakujalia huo, basi unaweza kwenda na uponywe. Amina.

249 Inakubidi kuliamini. Unaweza tu kufanya hivyo ukiamini. Ni wangapi wenu wanataka kuamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

250 Sasa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yeye amefufuka kutoka kwa wafu. Yu hai leo. Yupo hapa katika Kanisa Lake, akionyesha ya kwamba Kuja Kwake kunakaribia.

251 Ulimwengu utateketezwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Atomu tayari zimekusanyika pamoja katika—katika shehena na kadhalika, kuutia moto. Na, bali kabla ya hilo kutendeka, Mwana aliyeahidiwa atawasili, Mwenyewe, Yesu Kristo, kupeleka Nyumbani Kanisa Lake. Je! mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

252 Je! mnaamini kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanaamini sasa kwamba Uwepo Wake upo hapa, na unaamini kwamba alitoa tamshi hili, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya"? Inueni mikono yenu.

253 Sasa wekeaneni mikono mmoja juu ya mwenzake, mahali wagonjwa walipo, wekeni mikono yenu. Naam, nimechelewa, nahofia watanifanya nifunge. Weka, wekeni mikono yenu, sasa ombeaneni mmoja kwa mwenzake. Usijiombee mwenyewe, mwombee yule uliyeweka mikono yako juu yake. Sasa Yeye yupo hapa kuponya kila mmoja wenu. Aminini hilo!

254 Baba wa Mbinguni, tunaamini sasa kwa moyo wetu wote, kwamba katika Uwepo wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwamba ibilisi amepoteza nguvu zake, ushawishi wake, na Yesu Kristo anaishi sasa.

255 Ondoka, Shetani! Hebu watu hawa na waponywe, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu SWA64-0318
(Sir, We Would See Jesus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 18 Machi, 1964, katika Denham Springs High School kule Denham Springs, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org